For more visit : eazyarabic.com

102/3 MK
KCSE
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA
Aprili 2021

## THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

## KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

**Mwongozo wa Kusahihishia**
**(SIRI)**

**MWONGOZO HUU WA KUSAHIHISHIA NI MILKI YA BARAZA LA MITIHANI YA KITAIFA LA KENYA (KNEC) NA SHARTI KUREJESHWA KWA BARAZA HILI BAADA YA USAHIHISHAJI.**

**Mwongozo huu wa kusahihishia una kurasa 15 zilizopigwa chapa.**

© 2020 The Kenya National Examinations Council

(a) I.

(i) Mzungumzaji ni Mwalimu Mstaafu.

(ii) Anazungumza na hadhira ambayo imekuja kumuaga.

(iii) Yuko shuleni.

~~(iv) Ni katika sherehe za kumuaga.~~

**4 x 1 = 4**

II. Toni ya kuonya/ kutahadharisha -si vizuri kukitia kitumbua mchanga.

**1 x 2 = 2**

(Dondoo limetolewa uk. 121.)

III.

(i) Kuwadhalilisha wenzake kama vile Baraka, Festo, Mshamba na Nangeto anapoonyesha hali yao mbaya ya awali.

(ii) Kufichua njama za kifisadi – anasema pesa zilizochangishwa na rais zililiwa na wakora kama vile akina Festo.

(iii) Anapewa nafasi na Mwalimu Mosi kuhutubu lakini anamuaibisha anasema anafurahia kuondoka kwa Mwalimu Mosi.

(iv) Kutotambua mchango wa Mwalimu Mosi – anasema Mosi ataondoka shule ipumzike.

(v) Anashindwa kustahimili changamoto shuleni.

(vi) Anajidhalilisha kwa kusifia suala kama vile utapeli na wizi, hajiamini – anajiita zumbukuku asiyeweza kuimarika.

(vii) Anakosa kuyawajibikia maisha yake. Anamlaumu Mwalimu Mosi, anasema umaskini wake ulisababishwa na Mwalimu Mstaafu.

(viii) Anakosa kuwajibikia familia yake. Hatekelezi majukumu yake kama mume na mzazi.

(ix) Kutelekeza familia – hakuwahi kupita kwa Mwalimu Mosi kuwajulia hali wanafamilia yake. (uk. 128)

(x) Kumharibia Mwalimu jina kwa kusema kuwa amekioa kitoto chake. (uk. 130)

**~~10x 1 = 10~~: Kutaja $\frac{1}{2}$ Mifano $\frac{1}{2}$**

(b)

(i) Taswira – uoni – nyeupe, nyembamba

(ii) Tashihisi – mvi kujianika

(iii) Takriri/urudiaji – Alijaaliwa mvi

(iv) Tashbihi – kama theluji

(v) Taashira – mvi – ishara ya hekima

(Dondoo limetolewa uk. 120) **4 x 1 = 4**

2. (a)

(I)

(i) Haya ni maneno ya msimulizi.

(ii) Yanamhusu Sauna.

(iii) Sauna yumo nyumbani mwa Bi. Kangara.

(iv) Anahisi anakabiliwa na hatari fulani ndipo moyo unamwenda mbio.

(v) Anapofungua lango anakumbana na polisi ana kwa ana.

**4 x 1 = 4**

(Dondoo limetolewa uk. 153)

(II)

(i) Taswira hisi – anahisi / kikali

(ii) Mwendo - anatoka nje, moyo kumwenda mbio, kusimama

(iii) Usikivu – mbisho hafifu / anasikia

(iv) Mguso – vipapasio

**2 x 1 = 2**

(III)

(i) Tashbihi – anajihisi kama anayetarajia kuwa na kinyang'anyiro cha upiganaji masumbwi.

(ii) Tashhisi – kusimama kwa vipapasio vya akili / moyo wake ukimwambia.

(iii) Mdokezo wa methali- yake ya arobaini imefika.

(iv) Kutumia usimulizi wa wakati uliopo – mara anasikia…

(v) Nahau – kumwenda mbio.

**4 x 1 = 4**

For more visit : eazyarabic.com

(b)

(i) Kuonyesha changamoto zinazokumba hospitali za umma. Selume anashangaa namna alivyoweza kustahili matatizo kama vile ukosefu wa glavu hospitalini.

(ii) Kuangazia suala la ufisadi. Dawa zilizotengewa hospitali zinauzwa na wasimamizi wa hospitali. (uk. 140). Ruzuku kutolewa kwa wasiostahili.

(iii) Kuonyesha ukosefu wa uwajibikaji wa wasimamizi wa taasisi za umma. Hospitali haijalipia umeme. (uk. 140).

(iv) Kuendeleza ploti – kupitia sadfa. Kituo kinakamilika wakati ambapo Selume anajiuzulu; anapata kazi, na mkondo wa matukio kubadilika.

(v) Kuonyesha migogoro inayosababishwa na tamaa ya rasilimali. Mgonjwa analemazwa katika mapigano ya kung'ang'ania ardhi (141).

(vi) Kujenga tabia za wahusika. Kwa mfano, utu wa Ridhaa. Anaanzisha kituo cha afya na kuwapa ajira Selume na Kaizari.

(vii) Kuonyesha athari za matumizi mabaya ya vileo. Mwanafunzi anakufa kutokana na pombe haramu (uk. 142).

(viii) Kuonyesha ukengeushi. Wasomi wanashindwa kukabiliana na matatizo/ changamoto wanatumia mbinu hasi ili kujisahaulisha na hali yao duni (uk. 142).

(ix) Kuangazia changamoto zinazokumba sekta ya elimu. Halmashauri ya mikopo kutotosheleza mahitaji ya wanafunzi.

(x) Kuonyesha umuhimu wa mshikamano wa kifamilia katika maisha ya watoto. Kipanga anaingilia matumizi mabaya ya vileo kwa kukataliwa na aliyedhani ndiye babake.

(xi) Kuonyesha athari za kufuata mila zinazorudisha nyuma maendeleo ya kijamii. Tuama anakasirika kwa kupashwa tohara.

(xii) Kuaangazia suala la ukiukaji wa haki za watoto. Mama yake Pete kutoshughulika kutambua kwamba binti yake amekua na mahitaji yake yamebadilika.

(xiii) Kuonyesha jukumu la jamii katika kuwarithisha vijana mbinuishi. Mwanzo mpya inawapa vijana kama vile Kipanga huduma za ushauri nasaha unaosaidia kubadilisha tabia.

(xiv) Kuangazia uozo wa kijamii. Uavyaji mimba – Pete anajaribu kuavya mimba.

**10 x 1= 10**

3. (a)

(i) Nahau – kujitanua kifua

(ii) Mdokezo wa methali - mimi ni mwana wa mhunzi na bila shaka wa mhunzi asiposana huvuvia

(iii) Chuku - kuinua tani mia moja / kufufua maiti

(iv) Tashbihi / ulinganishi – kama yule mbabe wa kivita

(v) Balagha – angeweza kuinua tani ngapi vile za chuma?

(vi) Taswira – uoni- kuinua, wakitazama

(vii) Mbinu rejeshi – hadithi ya Fumo Liyongo na ile ya Akavi

(viii) Tabaini – si tofauti.

(ix) Udokezaji – anadokeza ushujaa wa Liyongo hatujui ni shujaa wa aina gani.

(x) Ubanaji wa matukio - Tukio linalotokea mara nyingi linasimuliwa tu mara moja.

(xi) Urudiaji – Baba, babangu.

(xii) Utata – matumizi ya neno hivi yanaweza kurejelea dhana zifuatazo:

- (i) namna
- (ii) kimchezo
- (iii) bila kusumbuka
- (iv) palepale
- (v) wakishangaa

(xiii) Kutumia usemi halisi na wa taarifa.

(Dondo limetolewa uk. 181)

**8 x 1 = 8**

(b)

(i) Kuendeleza mshikamano / ushirikiano wa kifamilia. Mwangeka na Mwangemi wanapendana. Wanashiriki shughuli mbalimbali.

(ii) Kuangazia historia ya jamii. Mwangeka anataja vita baina ya jamii yake na Akavi ili kuwaokoa mifugo. Kutajwa kwa mashujaa.

(iii) Kuangazia desturi / kuendeleza desturi kama vile utambaji. Nyanya anawahadithia kina Mwangeka kuhusu Fumo Liyongo.

(iv) Kusuluhisha migogoro/kuendeleza shughuli za usuhilishaji wa migogoro katika jamii. Babu Msubili ni jaji wa kienyeji.

(v) Kudhibiti vitendo vya wanajamii/kupitisha na kuendeleza imani za kijamii. Babu hakupenda kukutana na mwanamke asubuhi. Mama ya msimulizi anawakataza kumpelekea uji asubuhi; anawatuma ndugu wake wa kiume.

(vi) Kudumisha nidhamu. Mwangeka na Mwangemi wanapomwiga Babu wanachapwa na Babu, kisha wanakatazwa chakula.

(vii) Kutoa mwongozo kuhusu namna ya kuishi. Mama Mwangeka na Mama Mwangemi wanakilaani kitendo cha kumwiga babu; wanawaadhibu zaidi ili kukomesha tabia hii.

(viii) Kudumisha mahusiano ya kijamii/kaida zinazoongoza mahusiano ya kifamilia. Mwangeka na Mwangemi wanamwiga Babu ili kumkumbusha kwamba anastahili kuwa mtani wao kama ilivyo desturi ya jamii yao.

(ix) Kuendeleza shughuli za kijamii, kwa mfano michezo ya watoto na uigizaji.

(x) Kuendeleza imani kuhusu majukumu ya kijinsia katika jamii. Mwangeka anapobeza kuwepo kwa shujaa wa kike (Mekatilili – uk. 179).
Kuonyesha Imani ya jamii kwamba shujaa wa kivita sharti awe mwanamume. Babu anamkumbusha Mwangeka kuwa wanaume hawalali mapema.

(xi) Kuendeleza mbinu za kijadi za urekebishaji tabia/ufunzaji wa maadili. Babu anatumia kichapo, ambacho ndicho njia pekee iliyoaminika kumshinikiza mtoto kutii.

(xii) Kuhimiza maridhiano. Mwangeka na Mwangemi wanawapa majogoo wao punje za mahindi pamoja na kuwakumbusha asiyekubali kushindwa si mshindani. (uk. 183)

**Hoja 12x1 = 12**

**Kutaja $\frac{1}{2}$ Mifano $\frac{1}{2}$**

For more visit : eazyarabic.com

4. (a) (i) Ni maneno ya Asiya/Mamapima.

(ii) Anawaambia Wanasagamoyo waliokutana sokoni.

(iii) Wapo kwenye lango kuu sokoni.

(iv) Pombe yake imemwagwa; anajutia matendo yake ya awali.

**4 x 1= 4**

(Dondoo limetolewa uk. 92)

(b) (i) Usambamba – Nilijua ninawaponza
nilijua ninawapunja

(ii) Tashhisi – Nilimezwa na tamaa.

**2x2 = 4**

**Kutaja – 1**

**Mfano – 1**

(c) Ploti

(i) Kupitia kwake tunaelezwa kuhusu usuli wa utoaji wa kandarasi ya uokaji keki; yeye na Ngurumo walimwandama Husda.

(ii) Baadhi ya matukio katika maisha ya wahusika fulani yanaangaziwa katika kibanda chake cha pombe. Ngurumo anasema alisoma na Tunu (uk. 57) Tunaonyeshwa kuwa Siti alikuwa mlevi hapo awali. (uk. 58)

(iii) Wimbo anaoimba Mamapima ni kipengele cha ploti. Anautumia kuitetea kazi yake (uk. 60).

(iv) Anajenga mgogoro kati ya wanamabadiliko na wanaotaka hali ibakie hivyo. Tunu anasema amekuja kuwakomboa walevi ilhali Mamapima anasema anaharibiwa biashara.

(v) Matukio kwenye biashara yake yanawezesha kujua nani aliyempiga na kumuumiza Tunu. Ngurumo anaashiria miguu ya Tunu iliyoumia – (uk 63).

(vi) Kuonyesha hatima ya mgogoro baina ya viongozi na wanyonge. Anasema wamemgeuka, wameimwaga pombe.

(vii) Kuonyesha mustakabali wa Sagamoyo. Anajuta, anaomba msamaha; anaonyesha kuibadili nia/kueleza uanimifu wake kwa Tunu; anataka kuibusu miguu ya Tunu (uk. 92).

**~~6 x 1= 6~~**

**Kutaja $\frac{1}{2}$ Mfano $\frac{1}{2}$**

Maudhui

(i) Anaendeleza suala la ufisadi. Anapewa kandarasi ya kuoka keki kwa kuwa yeye ni rafiki ya Husda. Anahusiana na Ngurumo kimapenzi.

(ii) Kuonyesha upujufu wa maadili. Anahusiana na Ngurumo kimapenzi.

(iii) Kuonyesha ukosefu wa uwajibikaji. Anauza pombe haramu huku akijua ni hatari.

(iv) Anaangamiza kizazi cha vijana. Kwa kuwanzia dawa za kulevya (Mtu i, Mtu ii wameathirika na matumizi ya dawa za kulevya) (uk. 62)

(v) Anaonyesha matumizi mabaya ya cheo. Anapewa kibali cha kuuza pombe haramu kwa sababu mumewe ni kikaragosi cha watawala.

(vi) Anaonyesha haja ya maridhiano. Anajutia matendo yake, anaomba msamaha na kumtambua Tunu (anataka kumbusu).

(vii) Kuangazia mabadiliko. Anajutia aliyotenda. Anajiunga na wanaotetea mabadiliko.

(viii) Anaendeleza maudhui ya tamaa na ubinafsi. Anauza pombe haramu bila kujali athari zake kwa jamii. Kumweka Husda kwapani ili anufaike.

**6 x 1 = 6**

**Kutaja $\frac{1}{2}$ Mfano $\frac{1}{2}$**

5. (a)

(i) Wanachangia kuendeleza uchumi. Hata wanapokosa ajira, wanajiajiri. Sudi anachonga vinyago; Ashua anauza mandazi.

(ii) Wanapigania haki za wanyonge. Tunu na Sudi wakiwa chuoni walikuwa viongozi wa harakati za kupigania haki.

(iii) Wanawazindua Wanasagamoyo kuhusu haja ya kuwa na uongozi unaozingatia misingi ya kidemokrasia. Tunu na Sudi wanawahamasisha Wanasagamoyo kuhusu haki zao.

(iv) Wanaukosoa uongozi. Tunu anamkabili Majoka na kumwambia kwamba Wanasagomoyo wana haki ya kuishi (uk. 45).

(v) Wanahimiza haja ya kuzingatia maadili ya kijamii. Ashua anaheshimu asasi ya ndoa. Anakataaa ushawishi wa Majoka. Anakataa kufanya kazi katika shule ya Majoka inayowadidimiza watoto katika matumizi ya dawa za kulevya.

For more visit : eazyarabic.com

(vi) Wanachangia kuboresha hali ya utendakazi katika taaluma zao. Walimu wanagoma ili kupata mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

(vii) Wanatoa kielelezo cha uongozi ufaao. Tunu anasema kwamba wanahitaji viongozi wanaofahamu matatizo yao.

(viii) Wanafunza kuhusu umuhimu wa familia na malezi. Sudi anamwambia Ashua awafikirie watoto wao (uk. 48).

(ix) Wanaunda na kuimarisha itikadi za kijinsia zinazowawezesha kuleta mabadiliko katika jamii. Licha ya Sudi na Tunu kushukiwa kuwa wapenzi, hawalegezi juhudi zao za kuuhamasisha umma. Sudi anachonga kinyago cha mwanamke.

(x) Kuwakosoa wanyonge ambao wanatumiwa kama vibaraka. Tunu anamuuliza Ngurumo kipi muhimu; dhifa au kufunguliwa kwa soko. Sudi anawatanabahisha kina Boza kuhusu suala la majitaka.

(xi) Baadhi yao wanaendeleza ubaguzi wa kijinsia. Ngurumo anasema hawezi kumpa mwanamke kura.

(xii) Wanasisitiza umuhimu wa elimu na ustaarabu. Ashua anasema kutoelemika kuna tatizo (uk. 28), naye Husda anasema elimu bila ustaarabu haifai.

(xiii) Baadhi wanakwamiza juhudi za kupigania haki. Ngurumo anatumiwa na Majoka kumpiga na kumnyamazisha Tunu.

**10 x 1= 10**

**Kutaja $\frac{1}{2}$ Mfano $\frac{1}{2}$**

(b)

(i) Kuendeleza mgogoro wa kinafsia. Majoka anasema kuna kilio kikubwa ndani kwa ndani (uk. 73).

(ii) Kuchimuza matukio ya awali; kwa mfano kuuawa kwa Jabali (uk. 73)

(iii) Kudokeza hatari iliyomngojea Majoka – mikono yangu imefungwa kwa minyororo (uk. 73).

Majoka kusema yuko katika safari ya jongomeo.

(iv) Kuonyesha udhaifu wa uongozi wa Sagamoyo. Majoka anamuuliza Daktari/Babu kama ndiye rubani wa ombwe hilo. (uk. 74)

(v) Kujenga sifa za wahusika. Tunasawiriwa tamaa ya Husda inayomfanya kuuza pombe haramu.

(vi) Yanaangazia usaliti katika ndoa. Majoka anakiri kuwa anampenda Ashua; hampendi mkewe Husda.

(vii) Kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii; Wanasawiriwa kama wasioweza kutegemewa. Majoka anasema hawashikiki.

(viii) Kuonyesha ukosefu wa uwajibikaji wa uongozi. Majoka anasema hajashika usukani (uk. 80)

(ix) Kuonyesha kuwa Wanasagamoyo wamezinduka. Majoka anasema wanaililia damu yake (uk. 79)

(x) Kuonyesha kwamba Sagamoyo haipigi hatua kimaendeleo. (uk. 81)

(xi) Kuonyesha suala la mgongano kati ya utawala wa Babu na ule wa Majoka. Majoka anasema kwamba athari ya chombo cha Babu/kinatikisa chake (cha Majoka) na kukifanya kutaka kuubadilisha mkondo.

(xii) Kumtanabahisa/kumsuta Majoka kuhusu uongozi wake, na kumwonyesha haja ya kubadilika. Babu anasema: Huoni kisima kimeingiwa paka na maji hayanyweki tena?

**10 x 1 = 10**

**Kutaja $\frac{1}{2}$ Mfano $\frac{1}{2}$**

6. (a)

(i) Akipanda harudi chini.

(ii) Hawezi kuporomoka / kuanguka.

(iii) Amepata mbinu za kuendelea kupanda (ameotesha makwezi).

(iv) Makao / mahali pake ni pale juu/mamlakani.

(v) Kushuka kwake si halali / ni haramu.

(vi) Huhukumiwa ila hubaki huko juu.

(vii) Haoni hatari wala wasiwasi.

(viii) Amejishikiza penye manufaa.

(ix) Amepanga mikakati ya kujipatia pato.

(x) Hata mti ukiporomoka, hashuki.

(xi) Hata akipigwa vita, hashuki.

(xii) Atakatalia juu hata akipigwa na radi.

(xiii) Hashuki kwa hiari.

**6 x 1 = 6**

(b) (i) Taswira hisi – ukweli jua mchungu / yu furahani.

(ii) Taswira uoni – utabaki kutazama.

(iii) Taswira mguso – kagandama.

**4 x 1 = 4**

(c) (i) Urudiaji silabi / sauti – ngu, ngu, ngu (ubeti 1)

(ii) Urudiaji wa neno – tangu,tangu amepanda akapanda.

(iii) Urudiaji wa mstari / kipande - mpanda ngazi jamani.

**3 x 1 =3**

(d) (i) Kufinyanga sarufi / kubananga lugha- hili mja ubaini – ubaini hili mja, mengi mazao – mazao mengi

(ii) Inkisari – ngawiraye – ngawira yake / walo – walio.

**2 x 1 = 2**

(e) (i) Tanakuzi – mpanda – kushuka, juu – ardhini.

(ii) Chuku – mpanda ngazi kubakia pale miaka na dahari/ kushuka chini kuwa haramu.

(iii) Sitiari – mpanda ngazi – kiongozi anayepata mamlaka/ kilele kwenye mamlaka / ufanisi.

**3 x 1 = 3**

(f)

(i) Mistari minne katika ubeti.

(ii) Vipande viwili katika mishororo.

(iii) Vina vinabadilika kulingana na ubeti.

(iv) Mizani 8, 8 = 16 katika mshororo.

(v) Kipande cha mwisho cha ubeti kuanzia ubeti unaofuata.

**4 x ½ = 2**

7. (a)

(i) Alikuwa na uwezo wa kutenda mambo akiwa kijana, sasa hana.

(ii) Alikuwa na afya, sasa hana.

(iii) Alikuwa na ushirika wa ndugu na jamaa; sasa hana.

(iv) Anachoshika si chake – sasa hamiliki lolote.

(v) Amepoteza baadhi ya viungo alivyokuwa navyo. Sasa hana neno.

(vi) Vitamu ni vichungu kwake.

(vii) Hana la kumfurahisha kama awali.

(viii) Vilivyokuwa laini ni vigumu.

**5 x 1 = 5**

(b)

(i) Shairi lina beti tatu.

(ii) Kila ubeti una mishororo saba.

(iii) Kila mshororo una vipande viwili.

(iv) Vina vya ndani na vya nje vinatiririka.

(v) Mizani 8, 8 = 16 katika kila mshororo.

(vi) Kila ubeti unaanza kwa kauli; U wapi ujana wangu.

(vii) Kila ubeti unajitosheleza.

(viii) Kipande cha kwanza kinatoa wazo na cha pili kinakamilisha.

(ix) Shairi limetumia mistari kifu/toshelezi.

(x) Kila ubeti kuanza kwa swali la balagha.

**4 x 1= 4**

(c)

(i) Taswira hisi – machungu.

(ii) Taswira uoni – Tazama hii dunia.

(iii) Taswira mguso – laini, gumu,

(iv) Taswira muonjo – kitamu, kichungu.

(v) Taswira mwendo – nayo imeshika njia.

**4 x 1 = 4**

(d)

(i) Kweli kinzani - kitamu sasa kichungu

(ii) Tashhisi – afya imeshika njia

(iii) Tasfida – wamehama ulimwengu

(iv) Usambamba – Afya ya ujana wangu

siku ya ujana wangu.

**4 x 1 = 4**

(e) Nafsineni – mzee /mtu aliyekonga **1 x 1 = 1**

(f) Toni ya majuto/machungu/kukata tamaa – U wapi ujana wangu?

**1 x 2 = 2**

**Kutaja – 1**

**Mfano – 1**

8. (a) (i) Inaonyesha mwisho wa urafiki baina ya Sungura na Fisi- huo ukawa mwisho wa urafiki wa Sungura na Fisi.

**1 x 2 = 2**

**Kutaja – 1**

**Kufafanua – 1**

(b)

(i) Fanani kuzungumza moja kwa moja na hadhira – mjukuu wangu…

(ii) Matumizi ya chuku – mtu kujikwaa na mwingine kuwa ndiye anayehisi uchungu. Kuhitaji kutwa kujaza tumbo.

(iii) Tashhisi – Moyo wa fisi unamrai.

(iv) Methali – atanguliaye kisimani hunywa maji maenge. / Jikuna uipatapo

(v) Nahau – alishika tariki

(vi) Urudiaji – guu mosi, guu pili. / Takiri / uradidi

(vii) Ritifaa – Sungura anazungumza na Fisi na ilhali Fisi hayupo.

(viii) Tasfida – uwezo wa kuyatosheleza mumbile haja – badala ya – kwenda haja kubwa. Tauria

(ix) Kuigiza – alijikokota hivi …

(x) Swali la balagha – Itakuwaje … ?

Utaacha lini …?

(xi) Ucheshi – kicheko. cha Sungura

(xii) Tanakali za sauti – ndo ndo ndo!

(xiii) Taswira – fisi akilia. / Akishonwa

(xiv) Mtambaji kuhoji hali / upenyezi wa mtambaji – sijui kama mjukuu wangu …

(xv) Kuchanganya sauti ya usimulizi baina ya nafsi ya tatu hadi ya pili kupunguza masafa ujumi kati ya fanani na hadhira.

(xvi) Kuchanganya nyakati (uliopita na sasa) ili kupunguza masafa ujumi.

**10 x 1 = 10**

17. Kinaya – mtu kujikwaa na mwingine ndiye anahisi uchungu
18. Stihizai / kejeli / dhihaka – Sungura akicheka
19. Msemo – katika katakata
20. Nidaa/Siahi – Lo! Kiumbe huyu!
21. Uzungumzi nafsia – utaacha lini tabia hii ya usaliti
22. Tashbiha – Alijikokota mithili ya ng'ombe …
23. Usimulizi – Ndugu wewe unajua…
24. Taharuki – Hali ya kutaka kujua kitakachotokea
25. Dayolojia – Kati ya Sungura na fisi
K-10 x 1

(c)

(i) Kuashiria mwisho wa usimulizi.

(ii) Kuiondoa hadhira kwenye ulimwengu wa fantasia hadi ulimwengu halisi.

(iii) Kuwapa kitulizo wasikilizaji / kuwaondolea watu mwemeo wa matukio ya hadithini /~~kujua hatima ya tamaa ya fisi~~.

(iv) Kuonyesha mwisho wa mgogoro wa hadithini – unaashiria mwisho wa urafiki wa Fisi na Sungura.

(v) Kusawiri jamii ya fanani – ni wafugaji – anazungumza kuhusu ng'ombe.

(vi) Kuchochea wengine ili waweze kutamba hadithi.

(vii) Kusawiri mandhari ya jamii ya fanani.

(viii) Kuonyesha funzo la hadithi.

9. Kujua hatima ya tamaa ya fisi

**3 x 1 = 3** zozote 3

10. Kupisha shughuli inayofuata
11. Kupisha mtambaji anayefuata
12. Kujenga taharuki

(d)

(i) Kushiriki kwa kupiga makofi.

(ii) Kushiriki kwa kuimba nyimbo, ~~kutenda matukio mbali mbali ya hadithini na kuhuisha utamba~~ji.

(iii) Kuigiza baadhi ya matuko (matukio) /matendo ya wahusika. Kuhuisha utambaji

(iv) Kuuliza maswali/~~kujibu maswali.~~

(v) Kutoa mifano.

(vi) Hisia/wawazoonyesha (ishara na) usoni huweza kumfanya abadilishe uwasilishaji.

**(vii)** Kutoa – majibu kwa methali na vitendawili iwapo ngano itamalizikia kwa mtambaji kuwategea vitendawili.

(viii) Kutoa mifano ya baadhi ya wahusika wa hadithini kutoka jamii zao iwapo wataulizwa.

(ix) Wanaweza ~~kuchua~~ (kuchukua) nafasi ya kuitamba upya ngano hiyo.

**5 x 1 = 5**

10. Kutoa funzo katika hadithi
11. Kusikiliza – mh
12. Kucheka / Kulia
13. Kujibu maswali
14. Kunyamaza na kusikiliza kwa makini ili...